



**NIA ZA SALA ZA BABA MTAKATIFU  
ALIZOTOA KWA MTANDAO WAKE WA SALA ULIMWENGUNI  
KWA MWAKA 2026**

**JANUARI**

**Kwa ajili ya kusali na Neno la Mungu.**

Tusali ili kwamba kusali na Neno la Mungu kuwe kirutubisho kwa maisha yetu na chemchemi ya matumaini katika jumuiya zetu, hivyo kujenga Kanisa la kidugu na kimisionari zaidi.

**FEBRUARI**

**Kwa ajili ya watoto wenye magojwa yasiyo na tiba.**

Tusali ili kwamba watoto wanaougua magojwa yasiyotibika na familia zao wapate huduma ya kiafya na uangalizi unaohitajika, kamwe wasipoteze uimara na matumani.

**MACHI**

**Kwa upokonyaji wa silaha na amani.**

Tusali ili kwamba mataifa yaelekee kwenye kuacha matumizi ya silaha, hususan silaha za nyuklia, na kwamba viongozi wa ulimwengu wachague njia ya mazungumzo na diplomasia badala ya matumizi ya nguvu.

**APRILI**

**Kwa makasisi wenye changamoto**

Tusali kuwaombea mapadre wanapitia vipindi vya changamoto katika wito wao, kwamba wapate usaidizi wanaohitaji na kwamba jumuiya za watu zivasaidie kwa uelewa na sala.

**MEI**

**Kwa ajili ya upatikanaji wa chakula kwa wote**

Tusali ili kwamba kila mmoja, kuanzia wazalishaji wakubwa hadi walaji wadogo, wajitume kuepuka upotevu wa chakula, na kuhakikisha kila mtu anapata chakula bora.

## **JUNI**

### **Kwa ajili ya thamani ya michezo**

Tusali ili kwamba michezo iwe chombo cha amani, makutano na maelewano ya tamadui na mataifa mbalimbali, na iendeleze maadli mema kama vile heshima, mshikamano na makuzi ya watu.

## **JULAI**

### **Kwa ajili ya heshima ya maisha ya binadamu.**

Tusali ili kwamba maisha ya binadamu katika hatua zake zote yaheshimiwe na kulindwa, tukiyatambua kuwa ni zawadi kutoka kwa Mungu.

## **AGOSTI**

### **Kwa ajili ya uinjilishaji mijini.**

Tusali ili kwamba uinjilishaji katika miji mikubwa ambapo mara nyingi watu wanaishi katika hali ya kutojulikana na ya upweke, tupate njia mpya za kuitangaza Injili, huku tukibuni njia mpya za kujenga jumuiya za watu.

## **SEPTEMBA**

### **Kwa huduma ya maji.**

Tusali ili kuwe na usimamizi wa haki na endelevu wa maji, rasilimali muhimu, ili kila mtu aweze kuyapata kwa usawa.

## **OKTOBA**

### **Kwa ajili ya huduma ya afya ya akili.**

Tusali ili kwamba huduma ya kichungaji ya afya ya akili ianzishwe katika Kanisa lote, na kusaidia kuondokana na unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wenye magonjwa ya kiakili.

## **NOVEMBA**

### **Kwa matumizi mazuri ya mali.**

Tusali kwa ajili ya matumizi mazuri ya mali, kwamba pasipo kuvutia katika kishawishi cha ubinafsi, mali iwe daima kwa ajili ya manufaa ya wote na mshikamano na waliopungukiwa mali.

## **DESEMBA**

### **Kwa ajili ya familia zenye mzazi mmoja.**

Tusali ili familia zinazopitia kutokuwepo kwa mama au baba, kwamba zipate usaidizi na mwongozo katika Kanisa, zisaidiwe kubaki imara kiimani katika nyakati ngumu.

**Papa Fransisko**  
Vatikan, Desemba 31, 2024  
*Original: Italian*